



## Jifunze Kijerumani kupitia DW

Gundua lugha na utamaduni wa Ujerumani kupitia kozi za Kijerumani za mtandaoni bila malipo kutoka Deutsche Welle (DW).

DW imekuwa ikitoa kozi za kisasa na za aina mbalimbali za Kijerumani kwa zaidi ya miaka 60. Kozi za lugha mbili ni bora kwa wanaoanza. Wanafunzi wa kiwango cha juu wanaweza kuimarisha stadi zao kwa vipindi maalum, kama telenovela asilia. Uwe unapendelea kusoma maandishi, kusikiliza sauti zenye picha, au kutazama vidio, kuna kitu kwa kila mtu anayejifunza. Na kwa wale ambao wangependa kutumia kozi wakiwa hawako kwenye mtandao, kozi zenyewe zinaweza pia kupukuliwa.

[dw.com/kujifunzakijerumani](https://www.dw.com/kujifunzakijerumani)

## Audiotrainer

### Vipindi 100 vya kusoma msamiati



Lugha  
Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kirusi na Kihispania

Vifaa  
Karatasi za mazoezi na kitabu cha kazi  
(vinaweza kununuliwa kutoka [www.book2.de](http://www.book2.de))

Unaweza kujifunza msamiati ukitumia **Audiotrainer** ili kukusaidia kujua mambo ya msingi na kuimarisha vyema matamshi yako. Kuna vipindi 100 vya kukusaidia kujifunza jinsi ya kuuliza maswali na kujiamini katika maisha ya kila siku nchini Ujerumani. Kozi zote za lugha zinaweza kutumiwa mtandaoni au kupakuliwa kama jalada la MP3, au unaweza kujisajili kwa vipindi vyote kama jalada la sauti la mtandaoni. Audiotrainer inakuwezesha kujiendeleza kwa mujibu wa kasi yako mwenyewe.

[dw.com/kujifunzakijerumani/audiotrainer](http://dw.com/kujifunzakijerumani/audiotrainer)

## Deutsch – warum nicht?

### Kozi bora ya lugha kwa sauti



Lugha  
Kijerumani, Kiingereza na lugha nyingine 26

Vifaa  
Maandishi na daftari la mazoezi kwa ajili ya kuchapisha

**Deutsch – warum nicht?** Inasimulia kisa cha Andreas katika awamu nne – mwanafunzi anayefanya kazi kama mlinzi wa mlangoni kwenye hoteli.

Kila awamu ina vipindi 26 vinavyoweza kupakuliwa, ambavyo vinavyojumuisha mazungumzo, ufafanuzi wa sarufi, mazoezi, na jalada la sauti. Kozi ni ya lugha mbili, kwa hivyo unaweza kujifunza Kijerumani bila tatizo katika lugha unayoifahamu. Inapatikana katika lugha 28 tofauti.

[dw.com/kujifunzakijerumani/warumnicht](http://dw.com/kujifunzakijerumani/warumnicht)

## Deutsch Interaktiv Kozi ya kujifunza mwenyewe mtandaoni



Lugha  
Kijerumani, Kiingereza, Kirusi

Vifaa  
Mazoezi shirikishi, kamusi, vifaa vya sarufi,  
karatasi za mazoezi na vidokezo vya mafunzo

**Deutsch Interaktiv** hutoa mazoezi, majalada ya sauti, vidio, na picha mbalimbali ili kufanya mafunzo yavutie. Muhtasari wa sarufi na kamusi yenye zaidi ya maneno ya msamiati na vidokezo vya matamshi 7,000 hurahisisha mafunzo zaidi. Jisajili bila malipo ili kujijengea jina lako mwenyewe kwenye mafunzo. Programu inahifadhi matokeo yako na kukuongoza kwenye kozi hii. Kwa njia hii, unaweza kupanga wakati wako wa kujifunza ili ukidhi mahitaji yako vyema.

[dw.com/kujifunzakijerumani/deutschinteraktiv](https://www.dw.com/kujifunzakijerumani/deutschinteraktiv)

## Jojo sucht das Glück Tamthilia ya kujifunza Kijerumani




Lugha  
Kijerumani

Vifaa  
Mazoezi shirikishi, hati zenye vifaa vya msamiati, karatasi za mazoezi na vidokezo vya somo kwa walimu, karatasi za ukutani na milio.

Jifunze Kijerumani kwa njia tofauti kabisa kupitia **Jojo sucht das Glück**. Misimu mitatu, kila mmoja ukiwa na matukio 33 ya kuisisimua na mazoezi shirikishi, itakusaidia kuimarisha stadi zako za lugha kwa njia rahisi na ya kufurahisha. Ni nani angelidhani kuwa Kijerumani pia kingeweza kuwa lugha ya mapenzi?  
Jiunge na Jojo kutoka Brazil akitafuta furaha, maisha na mapenzi katika mji wake mpya, Cologne!

[dw.com/jojo](https://www.dw.com/jojo)

KUPAKUA  
BURE



Deutsche Welle | DW Akademie  
Bildungsprogramme  
53110 Bonn | Germany

[bildung@dw.com](mailto:bildung@dw.com)

© Deutsche Welle 2015

[dw.com/deutschlernen](http://dw.com/deutschlernen)